

## HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA

### UTARATIBU WA LESENI ZA BIASHARA, USHURU WA MALAZI(HOTEL LEVY),USHURU WA HUDUMA

S/N	AINA	UTARATIBU
1.	<i>Leseni ya Biashara chini ya Sheria ya utoaji leseni za biashara ya No. 25 ya mwaka 1972 na marekebisho yake ya mwaka 2014</i>	<p>Leseni ya kuhuishwa (Renewal) Mwombaji anatakiwa kujaza fomu ya maombi na kuambatanisha kivuli cha leseni iliyoisha muda wake. Leseni Mpya Mwombaji anapaswa kutekeleza yafuatayo:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>•Kujaza kikamilifu fomu ya maombi.</li> <li>•Kuambatanisha kivuli cha Namba ya usajili wa mlipa kodi (TIN).</li> <li>•Kuambatanisha uthibitisho wa uraia (kivuli cha cheti cha kuzaliwa, Passport ya kusafiria, cheti cha utaifa, kiapo Mahakamani , cheti cha kupiga kura.</li> <li>•Uthibitisho wa maandishi eneo la kufanya biashara.</li> <li>•Kama ni Kampuni ambatanisha nakala ya cheti cha usajili wa Kampuni na Memorandum and Articles of Association.</li> <li>•Kama ni jina la biashara aambatanishe vyeti vya usafili Brela (registration Certificate na Extract from Register).</li> <li>•Kwa mwombaji ambaye sio raia wa Tanzania aambatanishe kibali cha kuishi nchini daraja A.</li> <li>•Kama wenye Kampuni hawaishi nchini wanawakilishwa, waambatanishe hati ya kiwakili (power of Attorney).</li> <li>•Kwa waombaji wa biashara za Kitaalamu waambatanishe vyeti vya kuruhusiwa kufanya biashara hizo kutoka Mamlaka husika</li> </ul>
		<p>Makosa chini ya sheria hii</p> <ol style="list-style-type: none"> <li>i. Kuendesha biashara bila leseni hai na halali ya biashara.</li> <li>ii. Kushindwa kuweka leseni yake mahali pa wazi ambapo itaonekana.</li> <li>iii. Kushindwa au kukataa kutoa leseni ya biashara inapotakiwa na Afisa biashara au Afisa yeyote aliyeruhusiwa kisheria.</li> <li>iv. Kutumia leseni moja kuendesha biashara zaidi ya sehemu iliyoainishwa kwenye leseni.</li> <li>v. Kutumia leseni ya biashara eneo tofauti na lililoonyeshwa kwenye leseni.</li> <li>vi. Kutoa maelezo ya uongo ili kupata leseni</li> </ol> <p><b>ADHABU</b> Mfanyabiashara atakayetenda mojawapo ya makosa yaliyoorodheshwa hapa chini atakuwa ametenda kosa la jinai na adhabu yake ni kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi laki moja au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamaja</p>
2	<i>Leseni za vileo chini ya sheria No. 68 ya mwaka 1968 na marekebisho yake ya mwaka 1981</i>	<p>Waombaji wa Zamani Mwombaji ajaze fomu ya maombi na aambatanishe kivuli cha leseni iliyoisha muda wake. Waombaji Wapya Mwombaji ajaze kikamilifu fomu ya maombi na apitishe ngazi zote</p>

